

HAKI MBELE YA POLISI

Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA
(DESIGN AND DRAWING)
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA
NA ROYAL DANISH EMBASSY
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)

IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

HAKI ZA MTUHUMIWA MBELE YA POLISI

1. Mtuhumiwa ni nani?

Ni mtu yeyote ambaye anawekwa chini ya ulinzi na polisi au chombo cha usalama kwa kutuhumiwa kufanya kosa la jinai.

2. Makosa ya jinai ni yapi

Ni makosa ambayo mtu akipatikana na hatia hupe-wa adhabu.

Ni makosa kama wizi, ubakaji, mauaji, kufanya makosa ya kuhatarisha amani n.k.

3. Haki za Mtuhumiwa

- (a) Mtuhumiwa anapowekwa chini ya ulinzi ana haki ya kueleza sababu za kukamatwa au kutiliwa mashaka.
- (b) Mtuhumiwa ana haki ya kudai risiti ya orodha ya vyombo/mali atakayokuwa nayo wakati wa kumpekua zile zinazochukuliwa kituoni na pale anapokabidhiwa polisi.
- (c) Mtuhumiwa akiwa mwanamke lazima kukaguliwa na polisi mwanamke.
- (d) Mtuhumiwa ana haki ya kudai kibali cha hakimu pale majadiliano/maelezo kwa polisi yanapozidi saa nane.
- (e) Mtuhumiwa anayo haki ya kudai awasiliane na mtu anayemtaka akiwa chini ya ulinzi. Kwa mfano rafiki, ndugu au wakili.
- (f) Mtuhumiwa ana haki ya kufikishwa mahakamani katika muda usiozidi masaa 24.

- (g) Mtuhumiwa ana haki ya kukaa kimya wakati wa mahojiano na polisi na anapaswa kueleza kwamba chochote ambacho mtuhumiwa atawaeleza polisi inaweza kutolewa mahakamani kama ushahidi dhidi yake.
- (h) Mtuhumiwa ana haki ya kutojibu maswali ya polisi na kukaa kimya hadi polisi anayemuuliza/endesha mahojiano awe amemueleza mtuhumiwa yafuatayo:
 - (i) cheo alichio nacho na jina lake
 - (ii) mtahadharishwa kwamba yuko chini ya ulinzi.
 - (iii) kosa alilofanya au sababu ya kuwa chini ya ulinzi.
 - (iv) anayo haki ya kudai asomewe kilichoandikwa kabla ya kuweka sahihi kwenye maelezo.

Mtuhumiwa anayo haki ya kupewa heshima na kuthaminiwa kwamba ni binadamu. Hakuna ruhusa kumtesa mtuhumiwa na kumdhalilisha anayo haki ya kudai matibabu.

- (i) Mtuhumiwa anaweza akaomba dhamana wakati yuko chini ya ulinzi wa polisi.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Chama cha Wanawake wanasheria Tanzania TAWLA, S.L.P. 9460, DAR ES SALAAM.

